# AZIMIO LA EDINBURGH

## Kwa serikali za majimbo, miji na mitaa katika mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020

**31 Agosti 2020**

### Utangulizi

Sisi, serikali za majimbo, miji na mitaa – tukiwa washiriki na wachangiaji kwenye *Mchakato wa Edinburgh kwa Serikali za Majimbo na Mitaa katika maendeleo ya mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020*, na kutegemezwa na Sektretarieti na baadhi ya Wahusika katika Mapatano ya Bioanuwai (CBD) – ***tunahangaishwa sana*** na athari kubwa za kupungua kwa bioanuwai na mabadiliko ya mazingira katika maisha na jamii yetu. Tayari athari zinaonekana katika mazingira, miundo mbinu, uchumi, afya na ustawi wetu. Kwa kweli, janga la ulimwenguni kote la COVID-19 limetukumbusha jinsi ilivyo muhimu kuishi kwa upatano na vitu vya asili. Bioanuwai yenye afya na huduma za mfumo wa ikolojia inazotoa ni muhimu kwa ustawi wa binadamu na kujenga uimara wa miji na mikoa yetu, wakati wa na baada ya janga la COVID-19, na inapaswa kuwa sehemu muhimu ya kupata kwetu nafuu

***Tunahangaishwa*** kwamba, kama ilivyotajwa katika toleo la tano la ripoti ya Mtazamo wa Bioanuwai Duniani (GBO), hakuna yoyote kati ya Malengo 20 ya Bioanuwai ya Aichi (20 Aichi Biodiversity Targets) ambayo yametimizwa kikamili; kwamba utekelezaji wa Washiriki wa CBD pekee hautoshi kutuelekeza kufikia dira ya 2050 ya 'kuishi kwa upatano na vitu vya asili' au kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) ya Umoja wa Mataifa; na kwamba upatano miongoni mwa mikataba ya mazingira ya mataifa (MEA) unasonga kwa kiwango kidogo sana.

***Tunakubali*** kwamba *Ripoti ya Utathmini Duniani ya Bioanuwai na Huduma za Mfumo wa Ikolojia* ya IPBES imefikia mkataa kwamba, ijapokuwa utekelezaji mdogo, si kuchelewa sana kwa mazingira au bioanuwai, lakini utekelezaji huo wenye kuleta mabadiliko makubwa unahitajika katika ngazi zote.

***Tunatambua*** uhitaji wa mabadiliko makubwa katika mfumo wa ikolojia wa bahari na nchi kavu, na katika maendeleo ya miji na sekta zote zinazozalisha ili kuhakikisha kuimarishwa kwa usalama wa chakula, afya ya binadamu na ajira endelevu huku tukiepuka au kupunguza athari mbaya kwa bioanuwai. Pia, **tunatambua** jukumu la wenyeji wa asili na jumuiya katika usimamizi wa maeneo yao, ingawa uwezeshaji wenye matokeo wa bioanuwai kukubalika katika sekta zote.

***Tunatambua*** uhitaji wa kuunda sera, utawala na suluhisho la kifedha linalofaa katika ngazi zote za serikali na kuhakikisha uunganishaji wa sera katika ngazi ya kitaifa, majimbo, miji, na mitaa ili kuleta mabadiliko makubwa. Haya yanapaswa kushughulikia vichochezi vya moja kwa moja na visivyo vya moja kwa moja vya upungufu wa bioanuwai, na kuungaisha pande zote za maendeleo endelevu (kimazingira, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii).

***Pia tunatambua*** jukumu muhimu ambalo wenyeji wa asili na jumuiya, wanawake na vijana, mashirika yasiyo ya kiserikali, na jamii yote, katika ufanyaji wa maamuzi na utekelezaji katika ngazi ya jimbo, mji na mtaa, na kwamba kunapaswa kuwa na njia inayowahusisha wote ili kuhakikisha ushiriki wa vikundi hivyo.

***Tunakazia*** jukumu muhimu la sekta binafsi, kutia ndani sekta ya biashara, na ***kuzihimiza*** zichochee mabadiliko makubwa yanayohitajika kupitia kujihusisha kikamili, katika kuunga mkono uhifadhi wa bioanuwai, kurekebisha mfumo wa ikolojia na matumizi endelevu.

***Tunakazia*** jukumu muhimu ambalo serikali za majimbo, miji na mitaa zinatimiza tayari katika kulinda na kuongeza bioanuwai na katika kuleta utekelezaji kwenye upangaji, utimizaji na usimamizi.

***Tunaunga mkono*** uidhinishaji wa *Mpango wa Utekelezaji wa Serikali za Majimbo, Miji, na Mitaa kwa Bioanuwai (2011-2020)* chini ya Uamuzi X/22 na ***tunatambua*** jukumu muhimu ambalo hili limetimiza katika miaka kumi iliyopita kuhamasisha utekelezaji wa serikali za majimbo, miji na mitaa kuelekea malengo ya Mapatano; na kuchochea kutambulika zaidi katika jukumu muhimu la uungaji mkono wetu katika CBD.

***Tunaheshimu*** ahadi na kauli ambazo tayari zimetolewa na serikali za majimbo, miji na mitaa kutia ndani matangazo ya azimio[1,2] ya karibuni, na hasa matokeo yaliyopatikana kupitia mchango wa Mkutano wa tano na wa sita wa Bioanuwai Duniani wa Miji na Serikali za Majimbo – *Taarifa ya Quintana Roo Katika Kuhusisha Bioanuwai ya Majimbo na Mitaa* (2016) na *Taarifa ya Sharm El-Sheikh ya Utekelezaji wa Majimbo na Mitaa kwa Vitu vya Asili na Watu* (2018).

***Tunakubali*** uhitaji wa kujenga juu ya *Mpango wa Utekelezaji* uliopo chini ya Uamuzi X/22, na ajenda ya utetezi ya serikali za majimbo, miji na mitaa kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita, na ***kwa pamoja tunawajibika*** katika kuinua malengo na utekelezaji katika miaka kumi ijayo.

## Uundwaji wa mfumo wa bioanuwai duniani baada ya mwaka 2020

***Tunaunga mkono*** uundwaji wa mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020 hasa katika malengo ya wazi, yanayotegemea utekelezaji, SMART (Hususa, Yanayopimika, Yanayofikika, Yanayohusiana, Yanayopangiwa Wakati) na pamoja na mfumo wa usimamizi uliounganishwa.

***Tunashukuru*** Wenyekiti wa Kikundi Kinachoshirikiana Kisicho na Mipaka (Open-ended Working Group) katika mfumo wa bioanuwai duniani baada ya mwaka 2020 kwa kutumia njia inayohusisha na kushirikisha katika kuunda mfumo huo, na ***tunaunga mkono*** mbinu ya 'serikali nzima' iliyomo katika mfumo huo, ambayo inabeba kanuni ya uongozi katika ngazi zote za serikali, kutia ndani majimbo, miji na mitaa.

---

1 Aburra Valley – Medellin Declaration of Metropolitan Areas to the post-2020 global biodiversity framework (2019)

2 Carta de São Paulo - BIO2020 – Brazilian Perspectives for the Post-2020 Global Biodiversity Framework (2020)

Tunaendelea ***kuunga mkono*** dira ya 2050 "*kuishi kwa upatano na vitu vya asili"* na tuko tayari tukiwa na lengo kubwa la kutoa mchango utakaokuwa na matokeo katika ngazi ya chini hadi duniani kote, na kutoa mchango wa maana katika malengo ya muda mrefu.

***Tunashiriki lengo*** la Mkakati wa 2030 kama ulivyopangwa katika toleo la Maandishi ya Awali (Zero Draft) ya mfumo wa bioanuwai duniani kabla ya 2020, '*Kuchukua hatua ya haraka katika jamii yote ili kuelekeza bioanuwai katika kurejea hali yake ya kawaida kwa manufaa ya sayari na watu.'* Hili linahakikisha njia iliyo wazi kuelekea Dira ya 2050 na linapatana na lengo la serikali za majimbo, miji na mitaa kuelekea kushughulikia changamoto zinazohitaji kutatuliwa haraka duniani, kutia ndani mabadiliko ya hali ya hewa, kupunguza hatari ya majanga, afya na umaskini, pamoja na bioanuwai.

**Utekelezaji wa mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020**

***Tunaunga mkono*** uhusishaji wa serikali za majimbo, miji na mitaa, kama wawezeshaji muhimu wa utekelezaji wa mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020. Hata hivyo, ***tunatambua*** kwamba jukumu letu linahusisha zaidi ya kuandaa hali zinazowezesha.

Serikali za majimbo, miji na mitaa zina jukumu muhimu katika kuhifadhi, kurejesha na kupunguza hatari kwa bioanuwai, kutimiza mahitaji ya watu kupitia matumizi endelevu na kugawana faida kwa usawa, katika kuunda vifaa na suluhisho linatohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa hatua za kulinda bioanuwai, na kusimamia na kutoa taarifa.

***Tunatambua*** kwamba hatua tunazochukua katika kutekeleza na kufanya bioanuwai ikubalike huhakikisha kwamba utaratibu unaotegemeza na hali zinazowezesha ziko mahali pake katika ngazi ya majimbo, miji na mitaa – na kwamba uunganishaji wa njia ya uongozi utaongeza jitihada hizo.

***Tunakazia*** jukumu muhimu la serikali za majimbo, miji na mitaa katika kuandaa rasilimali kwa ajili ya hatua za utekelezaji na kufanya bioanuwai ikubalike. ***Tunakazia*** uhitaji wa jitihada za haraka na zenye kuongezeka ili kuandaa fedha katika ngazi zote za serikali na kutoka kwenye sekta binafsi.

Tuko katika nafasi ya pekee na inayofaa ya kuleta ufikiaji, ufahamu na matumizi ya mfumo katika jamii yote, kuwezesha ushiriki pamoja na wadau muhimu ili kutekeleza mfumo huo katika ngazi ya majimbo, miji na mitaa. Hata hivyo, ***tunatambua*** inawezekana kufanya zaidi katika sera na mifumo iliyopo tayari ili kuhakikisha jamii nzima inashiriki kikamili katika kuleta mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020.

**UJITOAJI KWA MFUMO WA BIOANUWAI DUNIANI BAADA YA MWAKA 2020**

Serikali za majimbo, miji na mitaa zitaendelea kujenga katika jitihada zilizopita, ili kuleta mabadiliko makubwa kwa:

- Kutambua thamani ya ujumla ya vitu vya asili na kuishirikisha katika mipango, usimamizi na vyombo vya uongozi vya serikali za majimbo, miji na mitaa;

- Kutekeleza hatua zinazofaa ambazo zinatimiza malengo ya mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020;
- Kuunganisha mikakati na utekelezaji wa bioanuwai, na jitihada zetu za kusimamia na kuripoti pamoja na Mipango na Mikakati ya Kitaifa ya Bioanuwai (NBSAP), ndani ya uwezo wetu wa majimbo, miji na mitaa;
- Kuongeza uandaaji wa rasilimali kwa ajili ya uwekezaji katika bionauwai katika ngazi ya majimbo, miji na mitaa, na kuandaa motisha itakayoleta matokeo mazuri;
- Kuwezesha bioanuwai ikubalike katika sekta za umma, binafsi na biashara ili kutokeza uimara wa kimazingira, uchumi, na kijamii;
- Kuwasiliana, kuelimisha na kuongeza ufahamu wa umma wa jitihada hususa za kufanya ujuzi upatikane katika lugha kadhaa;
- Kuimarisha mchakato wa kujenga uwezo ili kutekeleza suluhisho linalotegemea vitu vya asili (NBS) na maji na mimea, hasa kupitia njia zinazotegemea mifumo ya ikolojia na kuchangia kurejesha ufanisi kwa watu na sayari baada ya janga la COVID-19 (*green recovery*);
- Kuandaa nafasi za kubadilishana ujuzi katika ngazi zote za majimbo, miji na mitaa, na katika ya sekta zote katika jamii;
- Kushiriki mazoea bora katika ngazi zote za majimbo, miji na mitaa, ili kutekeleza kwa mafanikio hatua za mabadiliko;
- Kuleta muunganiko na mikataba na michakato ya serikali, kuendeleza hatua za kishujaa na kiubunifu katika ngazi ya jimbo, mji na mtaa ambayo hutokeza matokeo yenye kunufaisha wote.

**HIMIZO LA KUCHUKUA HATUA**

Sisi serikali za majimbo, miji na mitaa ***tunahimiza*** Wahusika wa Mapatano ya Bioanuwai;

I. Kuchukua hatua imara na za kishujaa ili kuleta mabadiliko makubwa, kama ilivyotajwa katika ripoti ya utathmini duniani ya IPBES, ili kusitisha upungufu wa bioanuwai.

II. Kutambua jukumu muhimu sana la serikali za majimbo, miji na mitaa, katika kutekeleza dira ya 2050 ya mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020, na mkakati wa 2030 kama ulivyoonyeshwa katika nyaraka ya Maandishi ya Mwanzoni (Zero Draft); na kuweka kwa uwazi utambuzi huo katika maandishi hayo ya mfumo, kutia ndani usimamizi wa mfumo kwa ajili ya malengo.

III. Kuunga mkono kurasimishwa kwa COP15, ya Uamuzi mpya kwa ajili ya uhusishwaji zaidi wa serikali za majimbo, miji na mitaa katika mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020; ambayo hujenga na kurudisha tena *Mpango wa Utekelezaji wa Serikali za Majimbo, Miji na Mitaa wa Bioanuwai (2011-2020)* kama ilivyoungwa mkono *chini ya* Uamuzi X/22*;* na hilo linaongeza kwa kiasi kikubwa malengo ya utekelezaji wa majimbo, miji na mitaa wa mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020 katika miaka kumi ijayo.

IV. Kuanzisha jukwaa la wadau wengi ili kuhakikisha uwakilishi wa serikali za majimbo, miji na mitaa katika kutegemeza utekelezaji wa mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020.

Sisi, serikali za majimbo, miji na mitaa, ***tuko tayari*** kukabiliana na changamoto ya utekelezaji,

pamoja na Wahusika, mfumo wa bioanuwai duniani baada ya mwaka 2020, kuhakikisha uwekezaji, na kutimiza jukumu zito katika kutekelezwa kwa mfumo kupitia *Mpango wa Utekelezaji wa serikali za majimbo, miji na mitaa* ulioboreshwa na kuongezewa nguvu katika miaka kumi ijayo.

**WASHIRIKI WA MCHAKATO WA EDINBURGH**

Bi Roseanna Cunningham, MSP

Katibu wa Baraza kwa Mazingira, Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Marekebisho ya Ardhi

Kwa niaba ya Serikali ya Scotland

Bi Lesley Griffiths AS/MS

*Gweinidog yr Amgylchedd, Ynni a Materion Gwledig*

Waziri wa Mazingira na Mambo ya Vijijini

Kwa niaba ya Serikali ya Wales

Bw Ashok Sridharan

Rais wa ICLEI

Kwa niaba ya ICLEI – Serikali za Mitaa kwa Uendelevu

Bi Cheryl Jones Fur

Naibu Meya wa Växjö, Sweden

Kwa niaba ya ICLEI Ulaya

Bi Elena Moreno

Rais wa Regions4

Naibu Waziri wa Mazingira wa Basque

Kwa niaba ya Mpango wa Maendeleo Endelevu wa Regions4

Bw Benoit Charette

Ministre de l'Environnement et de la Lutte

contre les changements climatiques

Kwa niaba ya Gouvernement du Québec

Bw Hideaki Ohmura

Gavana wa Wilaya ya Aichi

Kwa niaba ya Kikundi Serikali za Majimbo Zinazoongoza kuelekea Malengo ya Bioanuwai ya Aichi (GoLS)

Inafikiriwa

Kwa niaba ya Kamati ya Ulaya ya Mikoa

**Ikitegemezwa na:**

Bi Francesca Osowska

Mkurugenzi Mkuu

Kwa niaba ya NatureScot

Bw Simon Milne MBE

Mtunzaji wa Mfalme

Kwa niaba ya Royal Botanic Garden Edinburgh

**Ya tarehe: 31 Agosti 2020**

[Ukurasa Uliokusudiwa Kubaki Wazi]

**WATIA SAINI**

MAJIMBO, MIJI NA MITAA

| Jina | Cheo<br><br>Shirika | Tarehe Iliyotiwa Saini |
|---|---|---|
| *Mf. Jo Blogs* | *Mkuu wa Mgawanyo wa Mazingira na Vitu vya Asili*<br><br>*Baraza la Eneo* | *Xx/Mwezi/2020* |
| | | |

**WAUNGA MKONO WA ZIADA**

| Jina | Cheo<br><br>Shirika | Tarehe Iliyotiwa Saini |
|---|---|---|
| *mf. Nat Ure* | *Mkurugenzi, Shirika Lisilo la Kiserikali la Mazingira la Scotland* | *Xx/Mwezi/2020* |
| | | |

**Melekezo ya Kutia Saini**

Tunakaribisha kwa dhati ushiriki wa serikali za majimbo, miji na mitaa kutoka sehemu mbalimbali duniani katika kutia saini Azimio la Edinburgh; hivyo kuonyesha ujitoaji wao katika kuleta mabadiliko makubwa ili kutimiza azma na malengo yaliwekwa katika mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020.

Kwa kuongezea, kwa kutambua jukumu la, mf. mashirika yasiyo ya kiserikali na ya kibiashara, kuendeleza utekelezaji wa ngazi ya chini kwa ajili ya vitu vya asili, tunakaribisha uungaji mkono wa ziada wa mashirika kama hayo wa kanuni zilizotolewa katika Azimio la Edinburgh.

Wahusika wa Mapatano ndiyo wenye jukumu la kutimiza malengo ya dunia yaliyotolewa katika mfumo wa baada ya 2020. Ili kufikia mabadiliko makubwa ya kweli kwa ajili ya uumbaji wa asili, ngazi zote za serikali na jamii zinapaswa kufanya kazi zaidi kwa pamoja katika miaka kumi ijayo, hivyo tunakaribisha kwa dhati uungaji mkono wa Nchi yoyote Husika katika Mapatano ambayo ingependa kutambua – ingawa Azimio la Edinburgh – jukumu la waungaji mkono wa majimbo, miji na mitaa ndani ya mfumo wa bioanuwai duniani baada ya 2020.

Wote wanaotazamiwa kutia saini watapitia uhakiki mfupi ili kuthibitisha uwakilishi wao, na kuhakikisha wanagawiwa kundi sahihi:

i) Watia saini wa serikali za majimbo, miji, mitaa – mf. Waziri, gavana, meya, mkuu wa idara, wakuu wa miji, n.k.

ii) Waunga mkono wa Nchi Husika – mf. Waziri, mkuu wa idara, n.k., ndani ya serikali kuu inayounga mkono.

iii) Waunga mkono wa Ziada – mf. mashirika yasiyo ya kiserikali au ya biashara.

Wanaotazamiwa kutia saini wanapaswa kuwasilisha ombi lao kupitia;
enquiries-subnationalworkshop@gov.scot, ikiwa na kichwa **Saini ya ED**.

Ili kurahisisha mchakato wa uhakiki, inapowezekana tafadhali tumia anwani ya barua pepe ya shirika/rasmi (na sio anwani ya barua pepe ya kibinafsi). Tafadhali taja:

- jina,
- shirika,
- cheo ndani ya shirika,
- Ngazi ya uwakilishi (mf. wa kijimbo, kimkoa, kimji. kimtaa)
- Nchi
- Kundi la kutia sahihi ulilooomba, yaani. (i) - (iii) hapo juu

**Mfano:**

| | |
|---|---|
| **Jina** | Frederica Gonzales |
| **Anwani rasmi ya barua pepe** | F.Gonzales@madrid-council.es |
| **Cheo ndani ya Shirika** | Mkuu wa Mgawanyo wa Halmashauri wa Mazingira na Uumbaji wa Asili |
| **Shirika** | Halmashauri ya Madrid |
| **Ngazi ya uwakilishi** | Mji |
| **Nchi** | Hispania |
| **Kundi la utiaji saini** | Utiaji saini wa serikali za majimbo, miji, na mitaa |

Katika visa vya kutia saini kwa niaba ya mwakilishi au kiongozi, maombi yanapaswa kutia ndani ushahidi wa maandishi wa mamlaka ya uwakilishi huo ulioambatishwa na barua pepe ya maombi, mf. inaweza kuwa nakala iliyopigwa picha ya barua yenye nembo na anwani, pamoja na saini ya mwakilishi au ofisa.